**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI BUNGU

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu…………………..**

**Mkuu wa Shule 0713255403**

**Makamu Mkuu wa Shule 0716033113**

**Matron/Patron 0653789381**

**Shule ya Sekondari BUNGU**

**S.L.P 514 KOROGWE-TANGA**

**Tarehe 13/6/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA BUNGU SEKONDARI HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE MKOA WA TANGA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya HGK/CBG

Shule ya Sekondari Bungu ipo umbali wa Kilometa 60 Kaskazini/KMagharibi mwa Mji wa Korogwe Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Korogwe Nauli ni Shilingi **5,000/=** kwa basi, kwa pikipiki na Shilingi **15,000/=** na Tshs **30,000/=** kwa bajaji

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14/08/2023,** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni Sketi rangi ya oranji (karoti) mbili mshono rinda box iwe ndefu kuvuka magoti.
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu;
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) mbili nyeupe zifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (*ambatisha mshono*);
iv. Sare ya Michezo truck suit rangi ya light blue mbili.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule
vii. Sweta rangi ya damu ya mzee
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) gauni rangi ya kijani
ix. Tai ndogo fupi rangi ya oranji
x. Tisheti (T-shirt) rangi ya dark blue itapatikana shuleni

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari (*counter book quire 3 kumi* );
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro ft 3 inch 4. yanayotumiwa na wanafunzi wa bweni
vii. Mashuka Jozi 2 (light blue 1 na pinki 1*)*, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

**ANGALIZO**: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**b) Shule za Kutwa**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

**MUHIMU**

**Michango yote ya fedha iwekwe kwenye akaunti ya shule namba 41501100023 NMB BANK Jina la Akaunti ni Bungu Sec. Recurent Akaunt. Andika jina La mwanafunzi Katika Bank Pay Slip Upande wa mwekaji wa fedha. Mwanafunzi aje na Bank Pay Slip hiyo shuleni kuonyesha malipo aliyoyafanya**

**Mwanfunzi aje na vitabu vifuatavyo**

**HISTORY -** (a) Mastering History by Carto pp 1 & 2 b) (Major events in the world History by GervasZombwe (c) Advanced level History (form 5 & 6) oxford university press

**GEOGRAPHY** - (a) Contemporary issue in Geography by Msabila (b) Integrated approach Geography2 (c)Essential of practical Geography Advanced level (Form 5 & 6 ) (d)Economics and Human Geography 2

**KISWAHILI – Riwaya:** Vuta ni kuvute, Usiku utakapokwisha,Mfadhili na Barua ndefu kama hii.

**Ushairi:** Kimbunga, Na Chungu Tamu. **Tamthilia:** Nguzo mama, Kwenye ukingo wa thim, Morani

**DICTIONARY** – Kiswahili ya TUKI

**GENERAL STUDIES** - (a) A level General studies Notes

**CHEMISTRY** – ADVANCED PHYSICAL CHEMISTRY, ORGANIC CHEMISTRY PART A & B,INORGANIC CHEMISTRY 1 & 2 (MZUMBE BOOK PROJECT)

**BIOLOGY** – ADVANCED BIOLOGICAL SCIENCE, FUNCTIONAL APPROACH BIOLOGY

**REVIEWS** – HISTORY 1 & 2, GEOGRAPHY 1& 2, KISWAHILI 1&2, GENERAL STUDIES1&2.BIOLOGY 1& 2, CHEMISTRY 1&2 and PRACTICALS (BIOLOGY & CHEMISTRY)

***NB. VITABU HIVYO NI MALI YA MWANAFUNZI***

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0713255403**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0716033113**
- **Mwandamizi Taaluma 0718904563**
- **Mwandamizi Malezi 0653789381**